# UTAMADUNI NA ATHARI ZAKE KATIKA HARAKATI ZA UKOMBOZI WA MWANAMKE. MIFANO KUTOKA TAMTHILIA YA KIMYA KIMYA KIMYA NA KILIO CHA HAKI.

**NA:**

**NALUNJO AMELIA**

**21/U/15204/PS**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA KWANZA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MAKERERE**

**JULY 2024**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe. Haijawahi kutolewa na mtu yeyote kwa mahitaji ya shahada katika chuo Kikuu chochote. Haki zote zimehifadhiwa. Unakili wa tasnifu hii kwa mfumo wowote ule bila idhini yangu na chuo Kikuu Cha Makerere hauruhusiwi hata kidogo.

Saini.................................................... Tarehe....15/7/2024..........................

NALUNJO AMELIA

21/U/15204/PS

## IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa kibaki changu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo Kikuu Cha Makerere:

Saini.......................................... Tarehe....15/07/2024.........................

MSIMAMIZI: DKT. ARINAITWE ANNENSIA

CHUO KIKUU CHA MAKERERE

**SHUKRANI**

Kwanza namshukuru mwenyezi mungu kwa kunipa afya, uwezo na hekima kutekeleza utafiti huu. Shukrani nyingine za dhati kwa chuo Kikuu Cha Makerere hasa idara ya kiswahili na lugha nyingine za kiafrika kwa kunipa msingi timamu katika lugha ya kiswahili ambao umeniongoza hadi siku hii. Tena napitisha shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Arinaitwe Annensia kwa msaada na ushauri wake katika utekelezaji wa utafiti wangu. Mwenyezi mungu akujalie. Shukrani zisizo na kikomo kwa mamangu mpenzi Bi. Mary Kyokunzire kwa msaada wa kila aina. Asante sana mama kwa Kila jambo ulilonifanyia kuhakikisha kwamba naweza kutimiza ndoto yangu ya kumaliza masomo yangu katika chuo Kikuu. Safari hii haingewezekana bila ushauri wako na msaada wa kifedha. Naomba mwenyezi mungu akubariki na akuongezee miaka ili uweze kujivunia jasho langu. Shukrani nyingine ziwaendee walimu wangu walionifundisha na kunipa msingi thabiti katika lugha ya kiswahili. Wa kwanza ni Mwalimu Bwambale Moses aliyenifundisha kiswahili katika shule ya upili ya St. Mary's Vocational School, Kyamuhunga. Zisingekuwa nguvu zake, nisingefika kiwango hiki katika lugha ya Kiswahili. Shukrani nyingine ziwaendee walimu wangu katika chuo Kikuu Cha Makerere kama vile Dkt. Innocent Masengo, Dkt. Caesar Jjingo, Dkt. Mutungi Boaz, Bw. Kyomuhendo Victor, Bw. Nelson Nsereko pamoja na Dkt. Asiimwe Caroline. Najivunia kazi mlizonifanyia katika kutimiza ndoto yangu katika lugha ya Kiswahili. Naendelea kuwashukuru ndugu zangu kama vile Kaka Ntare Victor, dada zangu Nakaliika Maxencia na Nakiisekka Anicia, asanteni kwa msaada wenu. Mungu abariki kazi zetu. Mwishoni namshukuru rafiki yangu wa dhati Bi. Kenganzi Lynet  kwa yote aliyonifanyia wakati nilipokuwa nakumbana na maisha ya chuo Kikuu. Siwezi kuwataja wote kwa majina. Natambua mchango wa Kila mtu na naomba mungu awabariki.

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa, Bw. Ssemuli Freddie na Bi. Mary Kyokunzire, kama si nguvu zenu na hamu ya kuelimisha watoto wenu nisingejiunga na shule ya msingi, upili na chuo Kikuu wala kukamilisha masomo yangu.

## YALIYOMO

IKIRARI ........................................ **Error! Bookmark not defined.**

IDHINI........................................ **Error! Bookmark not defined.**

SHUKRANI........................................ v

TABARUKU ........................................ vi

SURA YA KWANZA; UTANGULIZI ........................................ 1

1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1 Usuli wa mada ........................................ 1

1.2 Tatizo la utafiti ........................................ 2

1.3 Malengo ya utafiti........................................ 2

1.4 Lengo kuu ........................................ 2

1.5 Malengo mahususi ........................................ 2

1.6 Maswali ya utafiti ........................................ 3

1.7 Umuhimu wa utafiti ........................................ 3

1.8 Upeo na mipaka ya utafiti........................................ 3

1.9 Hitimisho ........................................ 4

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI ........................................ 5

2.0 Utangulizi ........................................ 5

2.1Msingi wa Kinadharia........................................ 9

2.2 Ufeministi wa Kiafrika ........................................ 10

2.3 Mihimili ya nadharia........................................ 11

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................ 12

3.0. Utangulizi ........................................ 12

3.1 Eneo la utafiti........................................ 12

3.2 Vyenzo vya data ........................................ 12

3.2.1. Data za msingi........................................ 12

3.2.2 Data za upili ........................................ 12

3.3. Mbinu za ukusanyaji wa data ........................................ 13

3.4 Uteuzi wa sampuli ........................................ 13

3.5 Usomaji makini ..... 13
3.6 Uchanganuzi wa data ..... 13
3.7 Uwasilishaji wa matokeo ..... 14
3.8 Vifaa vya kukusanya data ..... 14
3.9 Kalamu na shajara ..... 14
3.10 Kompyuta ..... 14
3.11 Hitimisho ..... 14
SURA YA NNE: UTAMADUNI KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI NA KIMYA KIMYA KIMYA ..... 15
4.0 Utangulizi ..... 15
4.1 MUHTASARI WA KIMYA KIMYA KIMYA ..... 15
4.2 Tamthilia ya kilio cha haki ..... 18
4.3 Muhtasari wa tamthilia ya kilio cha haki ..... 19
4.4 MFUMO WA UTAMADUNI NA JINSI UNAVYOJITOKEZA KATIKA TAMTHILIA HIZI MBILI ..... 22
4.5 Tamaduni baguzi katika elimu ..... 23
4.6 Ubaguzi kazini/umaskini ..... 24
SURA YA TANO. CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA WANAWAKE KATIKA HARAKATI ZA KULETA UKOMBOZI ..... 24
5.1. Utangulizi ..... 24
5.1 Changamoto katika kazi husika ..... 24
5.2 Usaliti ..... 25
5.3 Matumizi mabaya ya mamlaka ..... 25
5.4 Mateso kwa wanawake ..... 26
5.5 Hitimisho ..... 26
SURA YA SITA ..... 27
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 27
6.0 Utangulizi ..... 27
6.1 Muhtasari wa matokeo ..... 27
6.2 Hitimisho ..... 28
6.3 Mapendekezo ..... 28
8.0. MAREJELEO ..... 30

# UTAMADUNI NA ATHARI ZAKE KATIKA HARAKATI ZA UKOMBOZI WA MWANAMKE. MIFANO KUTOKA TAMTHILIA YA KIMYA KIMYA KIMYA NA KILIO CHA HAKI.

## SURA YA KWANZA; UTANGULIZI

### 1.0 Utangulizi

Utafiti huu ulijikita katika mada ya utamaduni na athari zake katika harakati za ukombozi wa mwanamke katika tamthilia mbili ambazo ni Kilio Cha Haki (1981) na Kimya Kimya Kimya (2011). Ili kutimiza utafiti huu, mtafiti alichunguza data kutoka tamthilia mbili yaani kilio cha haki na kimya kimya kimya ili kupata data za kutimiza utafiti. Sura ya kwanza itaeleza juu ya vipengele vifuatavyo: utangulizi wa mada, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na hitimisho

### 1.1 Usuli wa mada

Hoppenau (2009) anafafanua utamaduni kuwa ni mfumo wa pamoja wa kiimani, maadili, desturi, tabia na kazi za Sanaa ambao hutumiwa na wanajamii katika kukabiliana na Dunia na Kati ya mtu na mwingine, unaorithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya kujifunza. Kwa mujibu wa (TUKI,2014), Mmwanamke ni mtu yeyote wa jinsia ya kike. Kimatumizi, neno mwanamke huashiria mtu wa jinsia ya kike aliye na utu uzima na aliyekomaa na kufikia umri wa kuolewa ilhali mwanamke mchanga au yule bado hajaolewa huitwa msichana katika tamaduni nyingi ulimwenguni (Hora, 2014).

Ukombozi ni jitihada za kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa ili watu wawe huru kwa haja ya mapambano dhidi ya wanyanyasaji. Ukombozi pia unaweza kuhusishwa na hali ambapo mtu binafsi anajikomboa kutoka kwa hali ya mateso au ya unyanyasaji. Yaani mtu ana uwezo wa kujikomboa kutoka kwa hali mbaya ya maisha inayomnyima haki yake au hata hali inayomdunisha.

Kadiri jamii inavyoendelea ndivyo mwanamke ametambua hali yake duni na kuanza kutafuta njia za kujinusuru kutoka katika hali hii. Mabadiliko haya yameonekana katika fasihi andishi ya kiswahili na ndiposa katika utafiti huu tunaangalia jinsi wanawake na ukombozi wao vinavyoathiriwa na mfumo wa kitamaduni ambao ni hasi kwa wanawake. Kwa kuangalia mabadiliko haya kwa upande wa wanawake, tutasaidiwa kwa kunukua mifano ya jinsi mipaka

ya utamaduni inavyoathiri ukombozi wa mwanamke kwa kurejelea mifano kutoka tamthilia zilizoteuliwa.

Kumekuwa na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali na asasi katika jamii kwa ajili ya kuleta ukombozi kwa wanawake. Jitihada hizo hutokana na kuwepo kwa ukandamizaji dhidi ya mwanamke katika masuala anuwai ya uhusiano wa kijinsia. Suala la kukosekana kwa usawa kati ya wanawake na wanaume si la bara la afrika pekee, bali limekuwako ulimwenguni kote. Suala hili limekuwa likihusishwa na utamaduni wa jamii husika. Tofauti kati ya nchi za kiafrika nan chi nyingine duniani ni kwamba, katika nchi kama marekani, ufaransa na uingereza, harakati za kuleta ukombozi zilianza zamani kwa kupitia dhana ya ufeministi ambayo badaye ilisambaa sehemu mbali mbali ulimwenguni.

Kulingana na usuli huu, utafiti huu utaangalia kwa upana dhana ya utamaduni na jinsi unavoathiri harakati za kumkomboa mwanamke katika jamii ya tamthilia mbili yaani kilio cha haki (1981) na kimya kimya kimya (2011.)

### 1.2 Tatizo la utafiti.

Tafiti nyingi za fasihi ya Kiswahili zimefanywa kuhusu ukombozi wa mwanamke kwa kuchunguza masuala kama vile elimu, dini na uongozi. Licha ya hayo, juhudi za mwanamke za kujikomboa na kupata hadhi katika jamii zimeangazia. Tafiti nyingi kama vile za Kimani (2003), Lugano (1985 na 1998) miongoni mwa wengine zimeonyesha kuwa mwanamke amedharauliwa kwa kupigwa, kutawishwa, kutukanwa, kubakwa na kadhalika bila kuangalia utamaduni kwa upana na undani katika kazi zao. Kwa hivyo, kinyume na tafiti za watafiti wa awali, utafiti wangu uliweka nguvu na msisitizo kwa kuchunguza suala la utamaduni na athari zake katika harakati za ukombozi wa mwanamke kwa kurejelea tamhtilia ya kilio cha haki (1981) na kimya kimya kimya (2011) kwa upana.

### 1.3 Malengo ya utafiti

### 1.4 Lengo kuu

Kuchunguza utamaduni katika tamthilia ya kimya kimya kimya na kilio cha haki.

### 1.5 Malengo mahususi

i) Kubainisha changamoto zinazowakumba wanawake katika kuleta ukombozi katika tamthilia ya Kilio cha haki na Kimya Kimya Kimya.

ii) Kuchunguza jinsi wanawake wanavyojikomboa dhidi ya changamoto zinasababishwa na utamaduni.

iii) Kubainisha athari za utamaduni kwa ukombozi wa mwanamke katika Kimya Kimya Kimya na kilio cha haki.

**1.6 Maswali ya utafiti.**

i) Je, utamaduni unaleta changamoto zipi katika harakati za kujikomboa kwa wanawake?

ii) Wanawawake wanakabilianaje na kutatua changamoto hizi? ii) Je, utamaduni una athari za aina gani kwa harakati za ukombozi wa mwanamke?

**1.7 Umuhimu wa utafiti.**

Utafiti huu utasaidia kwa kuonyesha wanawake jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba kwa sababu ya uwepo wa mipaka ya utamaduni inayomkandamiza mwanamke. wanawake watakaposoma kazi hii watawezeshwa kujua jinsi za kujikomboa wanapokumbwa na mipaka hasi ya utamaduni. Kwa kurejea kazi hii, itatoa mwanga kwa hadhira ya wanawake kuhusu jinsi ya kujinasua mtegoni wanapowekwa na utamaduni kwa kuangalia tamthilia mbili za kilio cha haki na kimya kimya kimya.

Kwa watafiti wa badaye watakaoshughulikia kazi inayohusiana na mada yangu, utafiti huu utakuwa wa muhimu sana kwao kwa kuwapa marejeleo ya kutimiza tafiti zao. Yaani baada ya kumalizika, utafiti huu utaweza kurejelewa na watafiti ili kuhakikisha maendeleo ya lugha ya Kiswahili na jamii kwa ujumla.

Kwa idara ya Kiswahili chuoni Makerere, kazi hii itasaidia wanafunzi wa Kiswahili katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwapa marejeleo ili waweze kuimarisha uelewa wao wa lugha ya Kiswahili. Kwa kuchunguza kazi mbali mbali za fasihi na kulinganisha hali katika tamthilia na ile katika jamii, wanafunzi hasa wa kike wanawezeshwa kubainisha jinsi ya kupambana na matatizo katika jamii zao kwa kurejelea kazi za fasihi.

**1.8 Upeo na mipaka ya utafiti.**

Utafiti huu ni wa aina ya maktaba na utajikita kwenye mada ya utamaduni na athari zake kwa ukombozi wa mwanamke katika tatmthilia ya Said A. Mohamed ambayo ni Kimya Kimya Kimya (2011) na kilio cha haki (1981) ya Alamin Mazrui. Utafiti huu ulifanyiwa katika maktaba ya chuo kikuuu cha Makerere wilayani kampala nchini Uganda kutoka mwezi wa Aprili hadi mwezi wa Julai. Uteuzi wa Maktaba hii ulifuatilia uwepo wa vitabu kadhaa, machapisho na magazeti kuhusu kazi za Kiswahili vitu ambavyo vilisaidia katika kutimiza utafiti wangu. Data katika utafiti huu zitakusanywa kutoka katika tamthilia hizi mbili ambapo

mitazamo na matendo ya wahusika wa kike vinavyolenga kuleta ukombozi vitachunguzwa kwa mbinu ya usomaji makini katika utekelezaji wa utafiti huu. Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya ufeministi.

### 1.9 Hitimisho.

Sura hii ilichunguza vipengele vifuatavyo: utangulizi ambaaao umetoa picha ya kijumla kuhusu masuala yatakapoangaliwa katika sura hii. Usuli wa mada umesaidia katika kutoa mwanga kuhusu kazi za watafiti wa awali na jinsi walivyochangia katika suala la utamaduni katika kazi zao na kunipatia mwelekeo na mwanga wa kutimiza utafiti wangu kwa njia ya kusaidia katika kugundua tatizo la utafiti. Tatizo la utafiti limesaidia kugundua shina ambalo linalengwa kuzibwa kupitia utafiti huu. Surah ii pia iliangalia vipengele kama vile maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na malengo ya utafiti na vimechangia katika utafiti huu kama nilivyoonyesha juu katika maelezo.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI.

## 2.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia maandishi ya waandishi na watafiti wa awali ambao walishughulikia suala la ukombozi wa mwanamke ambao kazi zao zinhusiana na mada yangu. Maoni ya wataalamu hawa yalilinganishwa na kujadiliwa kuhusiana na maoni yangu ili kutimiza kazi hii. Wataalamu hawa walishughulikia suala la ukombozi na utamaduni kwa upande wa mwanamke kwa njia zifuatazo:

Mugambi (1982) alihakiki maudhui katika tamthilia zilizochapishwa nchini Kenya kati ya mwaka 1957 hadi 1981. Kwa kutumia nadharia ya umaksi, Mugambi alionyesha jinsi waandishi walivyoendeleza maudhui mbali mbali kama vile udhalimu, nafasi ya mwanamke na utetezi wa haki za mwanamke. Kwa kuangalia tamthilia ya Zinduko (Ryanga, 1986), Mugambi alidai kuwa wanawake wamesawiriwa Kama viumbe duni ambao wanatumiwa na wanaume kuendeleza maslahi yao, viumbe dhaifu ambao hawana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao wanatarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa waume wao bila ukinzani. Anadai kwamba mwanamke katika tamthilia hii hana nafasi ya kuchangia katika siasa kama kiongozi bali jukumu lake ni kuwahimili wanaume. Utafiti huu ulichunguza taswira hii ya Mugambi kwa lengo la kubaini iwapo taswira hii inafana na ile ya mwanamke kiongozi katika tamthilia zilizotungwa tangu mwaka 2000 hadi 2016. Mugambi alitazama kuwa, Kilio Cha Haki (Mazrui, 1981) Ndiyo tamthilia ya kipekee ya Kiswahili iliyofikia kilele katika kubainisha hisia za ukombozi wa kijamii. Kulingana naye, tamthilia hii kando ya kubainisha mapambano ya wafanyikazi dhidi ya udhalimu, inatudhihirishia nafasi ya mwanamke katika jamii iliyo na mifumo kandamizi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lanina ambaye ni mhusika wa kike anajitokeza kama mwanamke jasiri aliyejikomboa kimawazo kuongoza mapambano ya wafanyakazi. Utafiti wa Mugambi ulifaa utafiti huu. Kupitia utafiiti wa Mugambi, picha mbali mbali za mwanamkeLanina ziliibuliwa na kuhusishwa na tamthilia teule. Picha hizi ni kama zile zinazohusu ujasiri, utetezi wa haki na msimamo thabiti wa mwanamke. Utafiti huu wa Mugambi ulichangia katika utafiti wangu kwa kusaidia kubaini namna lugha ya wahusika inavyochangia kujenga usawiri na taswira ya mwanamke.

Yego (2013) katika utafiti wake, alichunguza Nafasi ya mwanamke inayohusu juhudi za mwanamke za kupinga ukandamizwaji na kunyanyaswa kazini, kiuchumi na misingi ya kijinsia. Kulingana na Yego, mwanamke anaweza kujinasua katika hali hii kwa kupinga utamaduni usiomruhusu kujitengea nafasi yake katika jamii. Ninamuunga mkono Yego

kwasababu katika tamthilia ya kilio cha haki na kimya kimya kimya mwanamke ananyanyaswa na kunyimwa haki zake kwa sababu ya utamaduni wa jamii yake anamotoka. Kazi hii ilisaidia katika kulinganisha jinsi wanawake katika tamthilia nilizoteua wanavyokumbana na unyanyasaji katika jamii zao ili kupata uhuru wao

Lugano (1989) aliangazia wahusika wa kike katika kazi za Kezilahabi. Kazi hii ilisaidia kuonyesha kuwa wahusika wa kike wamechorwa kama viumbe duni na pia wao ni wanyonge. Alibainisha kuwa wahusika wa jinsia ya kike wameonyesha jitihadi za kujikomboa dhidi ya dhuluma wanazozipitia katika jamii zao wanamoishi. Kazi hii ya Lugano itaoanan na kazi yangu kwa sababu katika kazi yangu nitaangazia jinsi wanawake wanavyopambana na hali duni inayosababishwa na mfumo wa kiutamaduni katika jamii nyingi hasa zile za kiafrika na jinsi wanavyikabiliana na hali hiyo ili kufikia lengo lao la ukombozi kwa kuangalia vipengele vya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mbughuni (1982) alishughulikia usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili hasa katika riwaya zilizoandikiwa nchini Tanzania. Katika kazi zake, aligundua kwamba nafasi ya mwanamke nchini Tanzania ni hali ya chini ingawa chama cha TANU kilikuwa kinadhamiria kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume nchini Tanzania. Aliendelea kugundua kwamba katika uumbaji wa wahusika, wanawake walikuwa wanaendelea kuchorwa kama viumbe duni na kujitokeza kama wawakilishi wa maovu. Matokeo ya kazi ya mbughuni yatachzngia katika kazi yangu kwa kunipa marejeleo ya kulinganisha usawiri katika riwaya zile alizozingatia na usawiri katika tamthilia nilizoteua kutumia katika utafiti huu ambazo ni kimya kimya kimya (2011) na kilio cha haki (1981)

Karanja (1990) alihakiki tamthilia za Mzalendo Kimathi, Mkwava wa uhehe na kinjikitile na katika uhakiki wa kazi hizi, Karanja alibaini taswira ya kinifiu ya mwafrika katika vita vya ukombozi. Mtafiti huyu alionyesha jinsi Mwafrika alihusika katika vita vya ukombozi kwa mfano katika vita vya MAU MAU nchini Kenya tuliona kuwa mchango wa wanawake katika kuleta ukombozi wa nchi yao ulikuwa wa maana sana. Kwa hivyo utafiti wa Karanja utaniongoza nikiangalia jinsi mwanamke katika tamthilia ya kimya kimya kimya na kilio cha haki anavyochangia katika kuleta ukombozi wake dhidi ya unyanyasaji wake mwenyewe na uongozi mbaya wa jamii yake.

Fakih (2017) katika utafiti wake wa kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya mbili za Said. Muhammed yaani Utengano na Kamwe Si Mbali, alionyesha kwamba kuna tofauti ya usawiri wa mwanamke katika maisha ya zamani na usawiri wa mwanamke

katika maisha ya sasa. Naunga mkono mtafiti huu kwa sababu mwanamke wa sasa amebadilika na anajiamini kuliko wa zamani. Mwanamke wa sasa anaweza kuwa mwanajeshi, mwanasiasa, daktari, mwalimu, mbunge, kupata elimu anayoitaka na kadhalika jambo ambalo halikuwepo siku za zamani. Hivyo, ulikuwa mwongozo wa kunisaidia kuchunguza sifa anazopewa mwanamke katika tamthilia ya kimya kimya kimya na kilio cha haki.

Kiango (1992) ameangalia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Anasema kuwa mwanamke anaonyeshwa kama mtu ambaye hana usawa na mwanamme na pia kama kitega uchumi, mbaya, mzinifu, mtoaji mimba na mtupaji watoto. Anapohakiki tamthilia ya Kilio cha haki anasema kuwa inastahili kupewa nafasi ya kipekee kwa sababu mkabala wa Mazrui ni tofauti na waandishi wengine. Kazi hii itatusaidia kuendeleza maudhui ya ukombozi tukiona mchango wa wanawake wa kuleta ukombozi katika jamii. Nakubaliana na mtafiti huu kwa sababu katika jamii yangu mwanamke akichangia katika mambo ya siasa anatazamwa kama malaya, mwenye kejeli na mwizi. Utafiti huu utanisaidia sana nikichunguza mchango wa wanawake wa kuleta ukombozi dhidi ya mateso wanayoyapata wakijaribu kuleta ukombozi. Utafiti wangu utazingatia tamthilia ya Kigogo na Kimya Kimya Kimya na utachunguza mchango wa wanawake wakuleta ukombozi katika jamii yake.

Keter (2013) alishughulikia changamoto zinazomkumba mwanamke katika harakati zakujikomboa. Changamoto hizi ni pamoja na utamaduni, ndoa, wanawake kutoshirikishwa katika maamuzi, hali yakutojua miongoni mwa wanawake wenyewe, mfumo wa uchumi na ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa wanawake wenyewe. Keter alishughulikia nafasi mbili za mwanamke: hasi na chanya kinyume na watafiti wengine walioegemea upande mmoja tu. Utafiti huu utachunguza ikiwa nafasi chanya na hasi alizozizungumzia Keter zinajitokeza katika tamthilia za kimya kimya kimya (2011) na kilio cha haki (1981) na namna zinavyojenga kiongozi wa jinsia ya kike. Changamoto alizozibainisha zimewezesha utafiti huu kuchanganua mitazamo iliyopo kumhusu mwanamke.

Obure (2012) alishughulikia dhuluma zinazowakumba vijana wa kike katika riwaya mbili Rosa Mistika na Tumaini. Utafiti wake ulijihusisha na vijana wa jinsia ya kike pekee. utafiti wetu utaangazia uwezo wa wanawake katika kuikomboa jamii dhidi ya dhuluma wanazopitia. Vile vile katika jamii yangu, wanawake wanakumbwa na dhuluma nyingi na wanasimama kujikomboa dhidi ya dhuluma hizo na kwa hivyo utafiti huu utanisaidia kutimiza kazi yangu kwa kuirejelea nikichunguza dhuluma zinazowakumba wanawake katika tamtilia nilizoteua kwa mfano matusi, unyanyasaji, kupigwa na jinsi zinavyoathiri ukombozi wao dhidi ya mateso.

Ruto (2015) alitafiti kuhusu matatizo ya mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke na alieleza juu ya dhuluma mwanamke anazozipata kupitia maisha yake ya kila siku. Pia, alimsawiri mwanamke kuwa na matatizo mengi aliyokabiliana nayo yaani ndoa za lazima, dharau, kunyimwa haki za kuchuma mali na kurithi, dhuluma ya kimapenzi na kukengeushwa na jamii. Utafiti wangu unaafikiana na wa Ruto kwa sababu katika tamthilia nilizoteua, wanawake kama vile Mpya na Lanina walikumbwa na matatizo hayo na kujaribu kupigania haki zao na mwishowe wakajikomboa. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kugundua njia mwanamke anazoweza kutumia ili kupata suluhisho ya matatizo yanayowakumba.

Mwazani (2015) alifanya utafiti kuhusu maudhui ya ukombozi katika Diwani ya jicho la ndani. Katika utafiti huu alifafanua dhana ya ukombozi na aina mbalimbali za ukombozi katika Diwani hii. Utafiti huu ni wa muhimu kwa utafiti wangu kwa sababu utasaidia kuchunguza aina mbalimbali za ukombozi na jinsi zinavyojitokeza katika jamii na mazingira ya tamthilia ya kilio cha haki na kimya kimya kimya.

## 2.1Msingi wa Kinadharia

Mdee (2011) anaeleza maana ya nadharia kuwa ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Massamba Kama alivyonukuliwa na Msanjila (2006), alifafanua maana ya nadharia kuwa ni utaratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kielezo cha kuelezea jambo.

Hivyo basi, kwa kuwa nadharia ni dira na mwongozo utafiti huu utaongozwa na nadharia ya ufeministi. Nadharia ya ufeministi ndiyo itakayofaa utafiti huu kwa sababu waasisi wa nadharia hii walilenga kuangalia jinsi mwanamke anavyokumbana na hali mbaya inayomkumba ili kujikomboa mwenyewe na kupata uhuru dhidi ya mateso kama dhana yenyewe ilivyojadiliwa na wataalamu tofauti tofauti;

Ufeministi (kutoka mzizi wa Kilatini 'femina,' yaani wa 'kike'; au mwanamke. Kwa lugha ya kifaransa féminisme linamaanisha harakati ya ukombozi wa wanawake) ni jina linalojumlisha aina nyingi za misimamo, itikadi na matapo tofautitofauti yanayochangia lengo kuu la kutetea haki za wanawake dhidi ya ubaguzi wa jinsia uliotawala dunia kwa muda mrefu sana upande wa siasa, uchumi, utamaduni, dini na jamii kwa jumla (Luvenduski & Randall, 1993).

Evance (1995) alieleza kuwa nadharia ya ufeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko ulaya hususani nchini Uingereza na Marekani. Katika sehemu hizo, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbali mbali za kijamii kama vile kupiga kura au kuchaguliwa katika ofisi za uongozi. Hali hii ilionekana kama unyanyasaji dhidi ya haki za mwanamke na ndiyo ilikuwa chanzo cha mawazo ya kifeministi na nia ya kukomboa mwanamke kuepukana na hali hiyo. Nadharia hii ilianza kuzungumziwa Karne ya 19. Wakati huu, wagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao katika machapisho na kufichua matatizo yaliyowapata kama tabaka la kiuchumi na pia kama mwanamke. Wamitila (2002) alieleza kuwa baadhi ya kazi za mwanzo kuyafafanua masuala ya mwanamke kinadharia ni ''Avindication of the rights of a woman'' (1792) ya Mary Wollstonecraft. Pia, kazi nyingine ni ''The second sex'' (1952), ya Simone de Beauvoir ambaye alikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhahilisha mwanamke kama vile dini, ndoa na utamaduni. Wamitila na Simone de Beauvoir wanaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumbakiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo humfanya na kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Wamitila (2002) anaendelea kueleza kuwa uhakiki wa ufeministi wa kimarekani unahusishwa na kazi ya Mary Ellman, ''Thinking about woman.'' Dhamira kuu hapa ni kuonyesha jinsi

mwanamke anavyosawiriwa kwa namna mbali mbali katika kazi mbali mbali zilizoandikwa na mwanamume. Pia, mwandishi huyu alionyesha jinsi baadhi ya waandishi wa kike walivyoendeleza hali hii.

Wamitila (2003) alifafanua ufeministi kuwa ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Aidha, Wamitila aliongeza kuwa ufeministi ni nadharia ambayo inasaili na kudadisi itikadi ya kiume ambayo imekuwepo katika jamii kwa kipindi kirefu.

Ntarangwi (2004) naye alitoa maana ya ufeministi kuwa ni nadharia ambayo inajaribu kukiuka mitazamo ya kiume ambayo inatumiwa sana katika jamii. Aliendelea kusema kuwa nadharia ya ufeministi ilitokana na mkondo na harakati za kutetea haki za wanawake ulimwenguni na imejikita katika imani ya usawa wa kijinsia, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Williady (2015) pia alisema kwamba ufeministi ni nadharia iliyojaribu kuvunja mwiko wa mfumo dume hapa duniani kwa kuanzisha mapambano ya usawa wa kijinsia. Bila shaka majaribio haya bado hayajafanikiwa. Aliongeza kwamba hayajafanikiwa kwa sababu jamii inachukua muda mrefu kubadilika na kwahivyo matarajio ya wanawake yatafikiwa baada ya muda mrefu.

Kwa mujibu wa Barret (1988), ufeministi ni dhana inayoeleza hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ufeministi unapinga mfumo dume na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ambazo zinatawaliwa na wanaume.

Irib (2014) alieleza kuwa ufeministi ni harakati za ukombozi zilizoanzishwa na wanawake ili kupinga mfumo dume ambao unawakandamiza wanawake katika nyanja mbalimbali.\

Kulingana na usuli huu, kazi katika utafiti huu itaongozwa na nadharia ya ufeministi wa kiafrika kwa sababu misingi ya ufeministi huu inaafikiana na vitendo vya mwamko wa wanawake wanaolenga kujiletea uhuru wao wenyewe bila kutegemea wanaume kwa njia moja au nyingine.

### 2.2 Ufeministi wa Kiafrika

Mwasisi wa ufeministi wa Kiafrika ni Filomena Steady mnamo mwaka wa 1980 na kuendelezwa na Ogundipe katika mwaka wa 1994 ikiwemo waasisi wengine walioendeleza nadharia hii miaka ya 2004 hadi 2014. Filomena Steady alifafanua ufeministi wa Kiafrika kwa

kusema kuwa ni mapambano dhidi ya dhuluma na unyanyasaji wa wanawake yanayolenga kudhihirisha kuwa haki za wanawake zinatetewa na kuhifadhiwa.

Kwa idara ya Kiswahili, Kazi Steady inaweza kusaidia wanawake wanaosoma nadharia yake ili waweze kufunguka macho na kudai haki zao kwa kuwaonyesha jinsi ya kujikomboa wakikutana na changamoto kama vile ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa kielimu na ndoa za lazima. Kwa kuchunguza kazi mbali mbali za fasihi na kulinganisha hali katika tamthilia na ile katika jamii, wanafunzi hasa wa kike wanawezeshwa kubainisha jinsi ya kupambana na matatizo katika jamii zao kwa kurejelea kazi za fasihi.

### 2.3 Mihimili ya nadharia

Katika kushughulikia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika, ni bora kubaini kwamba kuna misingi ifuatayo ambayo ni ya kimsingi,

Nadharia hii inatumia fasihi kama jukwaa ya kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Msingi huu utakuwa nguzo kubwa katika utafiti huu ambapo tamthilia ya Kilio Cha Haki (1981) na Kimya Kimya Kimya (2011). Fasihi inarahisisha usambazaji wa ujumbe kutoka kizazi hadi kingine. Ndiyo maana tamthilia mbili yaani kilio cha haki na kimya kimya kimya ziliteuliwa ili kusaidia kwa kutoa sifa na matendo ya wanawake yanayodhihirisha harakati za kujikomboa dhidi ya mipaka hasi ya utamaduni.

Nadharia hii inalenga kuleta usawa wa kijinsia na kitamaduni kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii. Inapigania jamii mpya inayoheshimu jinsia ya kike kupitia amali zake. Kwa hivyo msingi huu unasaidia kwa kuonyesha kuwa mwanamke akijitahidi kupigania haki zake na ukombozi wake katika jamii, mipaka na minyororo ya kiutamaduni kama vile ubaguzi wa kijinsia katika elimu, kazi, ndoa za lazima na mateso kwa wanawake inayolemaza ukombozi wa mwanamke itavunjwa ili mwanamke aweze kujipatia ukombozi wake.

Nadharia hii hunuia kuzidua mwamko kwa upande wa wanawake kulingana na jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Msingi huu husaidia wanawake kugundua kwamba wakiamka na kuungana mikono, wenyewe wataweza kujisaidia ili kufikia lengo lao la ukombozi dhidi ya utumwa ambao umewabana kwa karne nyingi.

## SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

### 3.0. Utangulizi

Mbinu za utafiti ni utaratibu, kanuni na mwongozo ambao unatakiwa kufuatwa katika kufanya utafiti ili kuhakikisha kuwa data zinazopatikana zinakuwa sahihi na zinakubalika kitaaluma (kothari, 2008). Sura hii itaangalia vipengele muhimu vifuatavyo; mpango wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti, vyenzo vya data, ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data.

### 3.1 Eneo la utafiti.

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa tamthilia katika fasihi ya kiswahili. Fasihi ya Kiswahili inazo tanzu zingine kamavile: riwaya, ushairi na hadithi fupi. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) na Murumba (2011) tamthilia hujengwa kupitia matendo na mazungumzo ya wahusika. Utafiti huu ulijikita kwa utanzu wa tamthilia kwani ni kupitia matendo na mazungumzo ya moja kwa moja ya wahusika ndipo maudhui kama vile utamaduni zitakavyojidhihirisha ili tuweze kupata data za kutimiza utafiti huu. Imebainiwa kwamba nyingi za tamthilia hasa zile za kabla ya mwaka wa 2000 zilikuwa na mipaka ya utamaduni iliyomdunisha mhusika mwanamke (Onyoni, 2012; Murungi, 2013). Kwa niaba ya utafiti huu, nitachunguza mipaka hiyo na kubainisha athari za utamaduni huo kwa ukombozi wa mwanamke.

### 3.2 Vyenzo vya data

#### 3.2.1. Data za msingi

Data za msingi ni data halisi ambazo zinakusanywa na mtafiti kwa mara ya kwanza. Data hizo zitakusanywa kutoka tamtilia ya Kimya Kimya Kimya  na kilio cha haki huku nikichunguza dhana ya utamaduni kwa undani na kuangalia athari zake kwa harakati za ukombozi wa mwanamke.

#### 3.2.2 Data za upili.

Hizi ni data ambazo tayari zimekwisha kukusanywa na watafiti wa tangulizi na kuandikwa katika tasnifu, ripoti, nakala, vitabu, magazeti, majarida na machapisho pepe katika wavuti na tovuti. Data za upili zilikusanywa kwa lengo la kuniwezesha kama mtafiti kupata data za kusisitiza maarifa au kutolea msisitizo wa data za msingi.

### 3.3. Mbinu za ukusanyaji wa data

Kwa kiasi kikubwa utafiti huu utakuwa wa kimaktaba. Yaani sehemu kubwa ya utafiti huu itafanyika maktabani kwa kusoma tamthilia zote mbili zilizoteuliwa kufuatilia malengo na maswali ya utafiti ili kupata data za kutumia katika utafiti huu.

Uchanganuzi wa data za utafiti huu utafanywa kimaelezo ukiongozwa na malengo ya utafiti pamoja na nadharia ya ufeministi wa kiafrika.

### 3.4 Uteuzi wa sampuli.

Sampuli ya utafiti huu ni tamthilia mbili yaani Kimya kimya kimya (Mohammed, 2011) na Kilio cha Haki (Mazrui, 1981). Uteuzi wa tamthilia hizi ulifanywa kwa kufuatilia mbinu ya usampulishaji dhamirifu. Patton (1990) anaeleza kuwa kuna mikakati mbali mbali ya ushampilishaji dhamirifu. Kila tamthilia iliyoteuliwa iliafikiana na kigezo cha kuwa na mhusika mwanamke anayezungukwa na matatizo mengi katika jamii yake na kujaribu kujikomboa dhidi ya matatizo hayo.

Creswell (2003) anaibua fasili kuwa ushampulishaji dhamirifu ni mbinu ya usampulishaji ambapo mtafiti huteua sampuli kwa sababu inasaidia uelewa wa suala la utafiti na mada kuu ya utafiti. Kulingana na Mugenda (2003), mtafiti hutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu wakati anaposampuli kazi husika ambayo huwa na taarifa muhimu kwa utafiti wake kulingana na malengo yake.

### 3.5 Usomaji makini.

Kusoma Kwa makini ni kitendo Cha kuimakinikia matini Fulani ili kuweza kuelewa matini hiyo inazungumzia kitu gani (KombonaTrofrip, 2006). Katika utafiti huu, nilitumia mbinu hii katika kukusanya data za msingi ambapo matini yetu imekuwa tamthilia ya kimya kimya kimya (2011) na Kilio cha haki (1981). Kama mtafiti nilisoma tamthilia hizi mara kadhaa huku nikinukua data zinazohusiana na utamaduni wa jamii hizo mbili katika daftari ambazo nilitumia kudondoa data za utafiti huu. Hii mbinu ina umwafaka katika ukusanyaji wa data za kifasihi kwa sababu inawezesha mtafiti kukusanya data Kwa urahisi na uhakika huku akiwa tayari anajua ni nini anachokitaka huwa ni rahisi kukipata kutoka kitabu husika kilichoteuliwa.

### 3.6 Uchanganuzi wa data

Uchanganuzi utaongozwa na maswali na malengo ya utafiti kuonyesha namna mchango wa wanawake wa kuleta ukombozi unavyojitokeza katika tamthilia teule. Utafiti huu utaongozwa

na mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kuzingatia tamthilia ya Kigogo na Kimya Kimya Kimya.

### 3.7 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo yatawasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kurejelea malengo ya utafiti kama yalivyobainishwa katika sehemu ya malengo ya utafiti.

### 3.8 Vifaa vya kukusanya data

Kifaa ni kitu chochote ambacho kinaweza kutumika kufikia lengo fulani.

Utafiti huu utatumia vifaa mbalimbali kama vile kompyuta, kalamu na shajara ili kukusanya data maktabani. Vifaa hivi vitasaidia kunakili chochote kinachohusiana na mada ya utafiti wangu.

### 3.9 Kalamu na shajara

Ni vifaa vinavyotumika maktabani na uwandani. Katika kutafiti nitachukua mambo muhimu wakati wakukusanya data na kuyaandika kwenye shajara kwa kutumia kalamu. Kwa hivyo kalamu na shajara vitanisaidia katika kukusanya za kutekeleza utafiti wangu.

### 3.10 Kompyuta

Hiki ni kifaa muhimu katika kufanya utafiti kwani licha ya kuwa data za maktabani zimehifadhiwa humo, pia kitanisaidia kama sehemu ya maktaba ya kidigitali ambapo nyaraka zinazohusiana na mada hii pamoja na kupata maelezo kuhusu nadharia iliyotumika katika utafiti wangu, kupakua machapisho na maandishi ya awali kuhusu mada hii huwezekana. Kwa hiyo kompyuta ni kifaa chenye maana katika utekelezaji wa utafiti huu.

### 3.11 Hitimisho.

Sura hii ilibainisha kuwa utafiti huu ni wa kithamano uliojikita katika tamthilia mbili ambazo ni Kimya kimya Kimya (2011) na Kilio cha Haki (1981). Muundo wa uchanganuzi ulizingatiwa. Data katika tasnifu hii ilikusanywa kwa kupitia njia ya maktaba na kupangwa kisha kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Sura hii ilibainisha kuwa utafiti huu ni wa kithamano uliojikita katika tamthilia mbili ambazo ni Kimya kimya Kimya (2011) na Kilio cha Haki (1981). Muundo wa uchanganuzi ulizingatiwa. Data katika tasnifu hii ilikusanywa kwa kupitia njia ya maktaba na kupangwa kisha kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

## SURA YA NNE: UTAMADUNI KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI NA KIMYA KIMYA KIMYA

### 4.0 Utangulizi

### 4.1 MUHTASARI WA KIMYA KIMYA KIMYA

Tamthilia ya Kimya Kimya Kimya iliandikwa na Said.A. Mohamed mnamo (*2011)* nchini Tanzania. Tamthilia hii inazungumzia juu ya ubinafsi wa uongozi ambao umechukua muda. mrefu na ukaishia kuwaongoza vibaya wananchi kwa kuwadhulumu na kuwanyima haki zao. Wananchi wanaongozwa na Mpya katika harakati za kupigania haki zao, Mpya anampinga babake Bw. Binafsi. Wahusika wanaopatikana ni kama vile; Bw. Binafsi, Bi. Shoo, Mpwa, Mussa, zanga, Bw. Naona, Bw. Taja, Bw. Salimina, Bi. Mgeni, Bwa.Subira, Bw. Sikilivu, Mpishi, Fumbo, Kushoto, Kulia, Mkemeo, Wananchi na Sauti.Baadaye, anawaonyesha kidole Kulia na Kushoto na kuuliza kwani wanapeana na kusuguana migongo. Anaendelea kusema kuwa itakadi inakuja na dawa ya taifa ni uzalendo. Anawaambia ya kwamba, wanalazimika kuungana.

Mpya anaelekea kisimani, na kunywa bakuli la maji na kuwaonyesha wananchi kuwa anakunywa maji ya ujasiri kwa niaba yake na yao, anawaambia kuwa maji yanasafisha woga, baada ya kuyanywa maji, anajimwagia yaliyobaki, Kulia na Kushoto wanabagukana na kusema kuwa hakika nchi ni tamu kuliko siasa. Wote kwa pamoja wanakariri kauli kwa kusema eti ndio wa kujitolea mhanga.

Mkemeo ananyamazisha hadhira kwa msisitizo, katika familia ya Mzee Binafsi, Mpya anaonekana aneketi upande wake pekee, Mussa na Zanga upande mwingine, mama yao Bi. Shoo kwenye ncha ya meza, Bw. Binafsi hajaonekana, kiti chake kitupu. Vyakula vya kila aina vinaonekana mezani, wamemsubiri mwenye nyumba. Wakiwa hapo, chuma kinaanguka sakafuni ghafla kwa mpasuao mkali.

Mpya anasema kwamba chuma kimeangushwa lakini Sauti inamwambia eti kwao hawaruhusiwi kusema. Mpya anasema eti yeye ni mwananchi, mzalendo na mkereketwa ameanza. Vyombo vinammwagia ungao ambao unamfanya aseme.

Mpya anasema eti baba yake ni mtu wa ajabu na nafsi yake mwenyewe. Anaendelea kusema ati amechoka kusubiri, kungojea na kunyamaza, kwa sababu vinamkandamiza. Mamake Bi. Shoo aliyeketi katika ukingo mwennye hofu anataka kumsimamisha kusema lakini hawezi.

Baada ya muda, Bw.Binafsi anaingia na walinzi wake baada ya kuketi, yeye na Mpya wanatumbuliana macho. Bwa.Binafsi anamwamuru Mpya kuwa na adabu na kumkemea akimwita kigege na mtoto wa ukorofi. Anamwambia eti hakutaka mimba yake iingie. Mpya ankataa katakata kuinamisha kichwa. Baada ya hayao, Bw.Binafsi anawamuru kumwonyesha utiifu kwake. Mama yao Bi.Shoo anaanza na kumsihi kwa mapenzi yake. Zanga anafuata kwa wasiwasi kidogo na kuzungumzia utegemeo wake, anamshukuru kwa kuwatunza vizuri. Anasema kuwa baba yao ni kil kitu yaani, ni mwalimu wao, ni mganga wao, ni sheshe, ni padre na msema.Muda wa Mpya unapofika,hasemi bali anaguna wake na kumkumbusha juu ya vitendo vyake.

Bw.Binafsi anaamrisha walinzi kumburura, Bi.Shoo mamake anajaribu kumhurumia lakini anakatishwa na mumewe. Bi.Shoo anasema eti hawezi kumtupa mtoto wake na hivyo wanatoweka pamoja.

Zanga, Mussa na mama yao wanamrudia Bw.Binafsi baada ya suluhu isipokuwa Mpya. Wakati ni usiku wa mamane, Zanga amejilalia chumbani mwaka, halafu anaamshwa na Mussa kwa kugonga mlango. Zanga anaashiria kidole chake kinywani akimtarajia anyamaze. Mussa anapojaribu kumjibu alikokuwa na kwa nini anatoroka, anatumia Sauti ya juu. Zanga anamwambia kuwa anyamaze au atakiona cha mtema kuni. Mussa anamwambia kuwa wao wanaonyamazishwa lazima watoke na kuzitafuta haki zao za utoto- haki za binadamu. Haki aliyozaliwa nayo mtu, ya kusema pasi hofu na woga. Anaendelea kujiuliza mpaka lini atakuwa mtoto, ameamua kusema na ameamua kupiga kelele. Mpya sauti yake inawaambia eti kila kitu huanza kama mchezo yaani mwanzo wa ngoma ni lele. Mpya anaendelea kusema eti jambo hilo ni la kusema na kutetea haki za kila mtu. Onyesho linaishia tukiwaana wote wakisema eti wataungana na wanaojua kusema wawafundishe kusema kwa kuwa wanaojua kusema ni wengi kuliko wasiokujua kusema.

Wenye msimamo wa kusema na kupigania haki zao yaani Bw. Taja, Bi.Subira, Bw.Sikilivu, Bi.Mgeni, Mpya pamoja na wananchi wamekusanyika kwa Mkutano wa dharura. Katika mkutano huo, Bi. Subira kwa wazi anasema hana subira tena, yuko tayari kuyafichua yale yaliyofichika.

Bi. Subira anasema eti nchi imekaa kama msitu wa watoro, imejaliwa na waharifu. Wenzake wanamwunga mkono. Bi. Subira anawaelezea eti hawawezi kujikomboa bila ya kusema. Anasema vile vile eti nchini mwao, watu wanakata miti ovyo na kujenga nyumba bila vibali.

Aidha, viwanja vya watu vinachukuliwa kwa nguvu, kila pahali pamechafukika, anaendelea kusema kuwa uzalendo umefifia, wanauza nchi yao kwa bei rahisi…..

Bw.Taja anamwingilia kati na kusema eti orodha ni ndefu hawezi kuimaliza. Naye Bw.Taja anayataja yale yanayomwuma, akisema kuwa wamepoteza uraia na utaifa wao. Anasema kuwa wageni ndio wanaojaliwa na kuheshimiwa lakini wao wanaposema, hawasikilizwi.

Wakiwa wapo wanalalamikia mambo yasiyo na kikomo, kundi la wananchi linaloongozwa na Mpya linaingia. Mpya anawaambia kukomesha fujo kwani inaweza kuwaharibia mambo. Wananchi kwa ari ya kujikombo, wanasema kwamba hawatasita, hatakoma, wanasema mpaka kufa kwao.

Katika ofisi ya kiongozi mkuu ***(Bw. Binafsi)*** waziri wa nchi ***(Bw. Naona***) na ofisa wa usalama (***Bw. Salimina)*** wanaonekana humo. Bw. Naona hafichi mambo yoyote, anasema kinaganaga jinsi mambo yalivyo. Anapoulizwa kinachotokea Bw. Naona, anamwambia eti watu wameanza kuamka. Anaendelea kumwambia eti chini ya uongozi wake, watu wameamshwa na mengi na ni lazima wawe macho.

Pia, Bw. Salimina anapoulizwa jinsi anavyoona mambo, naye kwa msimano thabiti anamwambia kuwa watu wamekuwa wamelala na sasa wameamka, anaendelea kumwambia eti elimu aliyoisambaza ni ya uhange inayotukuza uongoza wake, na kwa hiyo wanataka wairekebishe katiba na waiandike upya. Bw. Binafsi anakasirika na kuanza kulipuka kwa maneno akiwadharau wananchi eti wamelala fofofo na wanalolijua ni kula mhogo. Anandelea akionyesha kuwa yeye ndiye kiongozi peke. Anauliza visababishi vya zogo.

Bw. Naona anamwambia eti mambo yalianzwa na Mpya, Mussa na Zanga watoto wake wenyewe ambao wamewaongoza wananchi. Bw. Binafsi anaahidi kuwa wakirudia vurugu hizo wakamatwe bila kumbagua yeyote wakiwa ni watoto wake au la kwani mtoto akililia wembe mpe, ukimkata ajuta mwenyewe.

Njiani, watu wanapiga huku na huku, wanasita kuisikia Sauti ya Mpya ambayo inasikika kokote ikisema kwamba wao wananchi wameamua kesho yake wakutane tena kulalamikia na kutetea haki zao. Sauti ya umma nayo inaendelea kusema ati hawatki na fujo bali inasikika ikikubaliana naye eti wako tayari kuingia barabarani na kusema kwa amani.

Mpya kwa utondoti anayesema wazi bila kuficha yatayoshughulikiwa kama vile, kupitia upya katiba yao, kusimama kidete kudai kugeuza mwendo wao wa kutojali masilahi yao,

kuhakikisha wananchi wanapata hunduma za kijamii, kupigana vita kwa ushujaa kuondoa ufisadi na kulinda rasilimali zao zinazoimbwa kiholera. Watu au wananchi wanakubaliana na kuvifanya hivyo.

Bw.Binafsi anaonekana amechanganyikiwa, anatembea huku na huku na kupiga hatua za masafa kama mwananajeshi. Anazisikia sauti za wananchi zikiimba wimbo wa mapinduzi. Anajaribu kuwanyanyamazisha lakini sauti zinamchekelea.

Anawauliza Bw.Naona na Bw.Salimina wakiwa wameshawapata wapigaji kelele kama walivyoagizwa. Bw.Naona anamwambia ukweli kuwa hawajawapata kwa sababu wamefichwa na umma lakini nyumba kwa nyumba na hatimaye watashikwa. Kwa ghadhabu, anawafukuza akisema hawezi kuvumilia, anawataka watoto wake kwa lolote.

Wananchi wanaonyesha kuwa wamejitayarisha na wako sawa kwa lolote. Bw.Binafsi anabaki katika ziwa la fikra na majuto yaliyojaa huzuni. Anaanza na kusema na yoo, analiomba limkejeli na kumsamehe yaani anaona amebaki peke yake kwa kuwa watoto wake wamemkimbia, watu wake wamemsusia na kumwendea kinyume. Yoo linamwambia eti lilimwonya lakini masikio akayatilia komango na kumdharau na hayo ndiyo matokeo yake. Bw. Binafsi anaanguka chini.

Nchi inanguruma Bw.Binafsi na Bi.Shoo wana jitimai na hofu wanapozisikia sauti za wananchi zinagonga kuta za nyumba. Sauti zao zinadai haki zao, wamesubiri miaka 50 lakini hakuna linalofanyika.Bi.Shoo anamwambia mumewe kuwa wameshamwambia kujiuzulu kwa masilahi ya nchi na umma lakini yeye bado anang’ang’ania, anaendelea kumwelezea eti wameshapoteza watoto wao, heshima udhibiti wao wan chi na hawawezi kusikilizwa na hawawezi kusilizwa na mtu yeyote. Baadaye, tunawaona wananchi wakiikabilia ana nguvu na kelele nyumba ya Bw.Binafsi. Bw.Binafsi anaonekana akijuta, mwisho wake umefika.

Hatimaye, tunawaona Kulia na Kushoto katika kufungio wakiimba kwa hoi hoi na nderemo. Wanafurahia mwisho wa utawala wa Bw. Binafsi. Wanaona lililobaki ni wananchi wenyewe kuisimamia nchi yao.

**4.2 Tamthilia ya kilio cha haki.**

Tamthilia hii iliandikwa na Alamin Mazrui mwaka wa 1981 kutoka nchini Kenya. Tamthilia hii inazungumza juu ya mapambano baina ya waafrika na wazungu. Wafanyakazi wa kiafrika wanaongozwa na mwanamke jasiri aitwaye Lanina na kupigana na makaburu uso kwa uso ili waweze kujikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni.

Vilevile, inafafanua kwa udhahiri jinsi mzungu anavyomtesa, kumdhalimu, kumyonya, kumyanyasa, kumtusu Mwafrika hivi kumyima haki zake. Baadhi ya wahusika wanaopatikana katika tamthilia hii ni kama vile: Delamon (kaburu mwenye shamba), Shindo na Zari ambao ni wasaidizi wake Delamon, Lanina ambaye anaongoza wafanyakazi katika harakati za ukombozi, Mwengo mumewe lamina, Baba ambaye ni babake Lanina, Mama ambaye anamzaa Lanina, Dewe, Musa, Makachero (1 na 2), Pelekha na Matovu ambao ni viongozi wa chama kipya cha wafanyakazi wa Delamon na wengine.

**4.3 Muhtasari wa tamthilia ya kilio cha haki**

**Onyesho la kwanza (uk7-14)**

Ofisini mwa Bwana Delamon ana wasaidizi wake Shindo na Zari. Wote hawa wanaonekana wamejaa wasi wasi na hasira kwa sababu ya malalamiko ya wafanyakazi ambayo yamejaa mezani kwa njia ya barua. Wafanyakazi wanapinga udhalimu na unyonyaji unaowatendewa na Bwana.Delamon. Sauti za wafanyakazi zinadhihirisha jinsi wanavyoteswa na mizigo mizito yahasira na uchungu.

Katika onyesho hili, Delamon anaonyeshwa akiwa na hasira nyingi sana kwa wasaidizi wake Shindo na Zari kwa kushindwa kumnyosha na kumkatiza Lamina kutoendelea na mipango yake ya uchochezi wa migomo dhidi ya udhalimu wa bwana Delamon. Katika ziwa la wasiwasi, Delamon anamwamuru Shindo kumpigia simu kamishna wa polisi Bwana Henderson ili amwelezee mengi kuhusu mgomo wa wafanyakazi. Shindo simu inamwanguka mikononi halafu Delamon anajishikia simu na kumpigia Henderson mwenyewe.

Baada ya simu, Lanina na Tereki wanakaribisha ofisini mwa Delamon. Delamon anawaagizia chai lakini wanaikataa kwa kusema hawana hamu. Delamon anajaribu kuwahoji juu ya chanzo cha uchochezi huo wa migomo lakini Lamina anakataa kuongea mengi na kudai kwamba malalamiko ya wafanyakazi yameshaletwa katika barua na hakuna haja ya kuyakariri. Sauti zawafanya kazi zinaendelea kusikika. Lanina na Tereki wanaelekea upande wa mlango.
Mlangoni wanakutana na askari polisi wawili na kuwatia pinguni.

***Onyesho la pili (uk15-20).***

Katika ofisi ya polisi, Shindo na Kachero wanaonekana wamekaa upande mmoja wa meza. Wawili hawa wanajaribu kuzungumza juu ya mpango wa bwana Delamon kwa wafungwa wake wawili waliofungwa kwa sababu ya uchochezi. Badaye, askari wawili wanamleta Tereki na kachero anamkaribisha kwa kumpa kiti ili akae. Shindo anajaribu kumsawishi ili akubaliane na maoni ya Bwana Delamon lakini anakataa. Shindo anamwelezea kwamba Delamon ni mtu mzuri aliyejaa huruma na ako tayari kumfa nyia kila atakalo ikiwa atakubali kuacha uchochezi wa migomo. Tereki anaomba apewe wakati wa kulifikiria Jambo Hilo. Baada ya hapo, Tereki anapewa siku mbili za kufikiri na halafu askari wawili wanarudi na kumchukua hadi chumbani mwake gerezani.

***Onyesho la tatu (uk21-28)***

Katika onyesho hili, Lamina anaoneka akiwa gerezani huku makachero wawili wakiendelea kumhoji na kumwonya dhidi ya kesi zake za kila siku. Kachero mmoja anamwambia kuwa hii ni mara ya pili akifungwa kwa kosa hilo hilo la uchochezi. Mara ya kwanza ilikuwa katika shamba la Rhodeman na mara ya pili katika shamba la Delamon.Kama kawaida, tunaona Lamina amekataa kushikiriana na wazungu. Anaendelea kuwaelezea kwamba mgomo si wake peke yake bali ni wa watu wote wanaodhulumiwa na wazungu nchini.

Lanina anateswa kwa kubinywa lakini anavumilia. Kachero anaendelea kumwuliza lamina lengo lake la kufanya huu uchochezi na kabla ya kulijibu swali hilo anapigwa kofi linalomwangusha chini. Kwa ujasiri Lamina anawaelezea kwamba madhumuni ya migomo ni wafanyakazi kupigania haki zao na kukomesha uongozi mbaya kama wanavyoimba katika nyimbo zao.

Mashawishi yote haya anayafanya kipindi anampapasapapasa kimapenzi lakini Lamina anamrukia na kumtusi kwa kumwita mhuni jambo ambalo linamhuzunisha sana kachero. Kachero wa pili anaendelea kumsawishi kwa kudai kwamba rafiki yake Lamina aitwaye Tereki ameshageuka mawazo na sasa ameungana na wazungu na amekwishapewa nyongeza na kurudishwa kazini. Baada ya kukataa, Lanina anaachiliwa uhuru na kuondoka huku akihisi maumivu kutokana na mapigo.

nyia kila atakalo ikiwa atakubali kuacha uchochezi wa migomo. Tereki anaomba apewe wakati wa kulifikiria Jambo Hilo. Baada ya hapo, Tereki anapewa siku mbili za kufikiri na halafu askari wawili wanarudi na kumchukua hadi chumbani mwake gerezani.

***Onyesho la nne (uk29-35)***

Nyumbani kwake Mwengo, anaonekana akivuta sigara katika chumba chake ambacho kinadhihirisha hali ya umaskini kulingana na jinsi kilivyopambwa. *Mwengo* anamfungulia mlango mke wake Lamina anayetoka kizuizini kwa mara ya pili kwa kesi zake za uchochezi wa migomo na harakati za kupigania haki zake na za wafanyakazi. Mwengo anamfokea mkewe kwa kumtia wasi wasi nyigi kwa muda alioumaliza kizuizini. Anamlaumu kwa kuacha familia yake mikononi mwa mume na kwenda katika mambo ya siasa zisizo na mbele wala nyuma. Lanina anamwambia mumewe apoe moto ikiwa anataka kuzungumza naye. Anaendelea kumbembeleza mtoto wake Dida na kwenda chumbani kumlaza. Anaporudi, anajaribu kumwelezea Lamina mumewe kila jambo. Mumewe anamhurumia baada ya kuona jinsi alivyoteswa kizuizini na makachero. Lanina anaendelea kumwelezea changamoto za wafanyakazi na yeye Mwengo mwenyewe akiwemo. Anamwelezea umuhimu wa kuungana mikono ili kupigania haki zao kama wafanyakazi. Mwishowe, Mwengo anakubali kujiunga na watetezi wa haki za wafanyakazi lakini kwa shingo upande. Halafu Mwengo anashikana mkono na Lanina na kwelekea chumbani kulala.

***Onyesho la 5(uk36-42)***

Katika familia ya baba na mama ambao ni wazazi wake lamina, Baba mtu anaonekana akiwa na hasira zisizo na kikomo kwa sababu ya vijana wa siku hizi hasa wale wa jinsia ya kike, anawalaumu vijana kwa Kuacha mila zao na kujaribu kuishi kama wazungu. Baba ana hasira kwa sababu Mwengo amemshataki Lamina kwa babake kwa madai kwamba hahudumii familia yake bali yeye anajiingiza katika mambo ya siasa ambayo yanaangaliwa kuwa ya wanaume. Kwa hasira, baba anafika kiwango cha kusema kwamba Lamina si motto wake. Mamake Lamina anajaribu kumtetea binti yake kwa kusema kwamba Lanina ana kazi mjini na watu wa kijijini huwa wanajaribu kumharibia jina kwa kumpaka sifa zisizomfaa hata kamwe.

Baada ya makabiliano hayo, Lanina anaingia kutoka kizuizini. Anakaribishwa na mamake anayemlilia kwa maisha magumu aliyoyapitia wakati alipokuwa kizuizini. Lamina anapojaribu kumsalimu baba, baba anamkaribisha kwa matusi na kumwonya kutomwita babake tena. Baba anajaribu kumfunza mkewe eti amfunze adabu binti yake. Baada ya hayo, mama anamkalisha na kumfunza adabu Lanina. Anamwambia kuwa mke sharti amtii mume wake, awe chini yake na amhudumie. Kwa ghafla, baba anajitokeza akishika bakora mkononi tayari kuwafunza adabu mama na motto wake. Anamkimbilia Lanina na nia ya kumpiga lakini kwa kudra za mungu Lanina anakimbia na kumwacha bila kupigwa huku mama kaanguka chini na kulia kilio cha kwikwikwi. Baba anamfukuza Lanina kutorudi nyumbani kwake.

*Onyesho la sita (uk43-48)*

Katika shamba la Delamon, wafanyakazi waliomo Tereki, Matovu, Dewe, Musa na mfanya kazi mwingine wana mivutano. Musa na Dewe wanataka kumtetea Lamina anayetetea haki za wafanyakazi wenzake. Mfanya kazi mwingine anasema kwamba wao wamepewa nyongeza jambo linalomlazimisha Musa kumwita mjinga. Tereki anamshabiki mfanyakazi mwingine kwa kudai kwamba pia wamepewa nyongeza. Mivutano inaendelea lakini Dewe ambaye ana nguvu nyingi za kimwili anawatenganisha.

**Onyesho la saba, nane na mwisho.**

Katika maonyesho haya tunawaona Tereki, Pelekha na matovu wanamtembelea Lamina ili kumliwaza kwa kufungwa kizuizini alimomalizia siku kadhaa. Lanina anawaelezea kwamba katika harakati za ukombozi, matatizo mengi huwa yanatarajiwa na nilazima wasimame imara. Lanina anakataa msaada wa Delamon kwa kusisitiza kwamba shida zao si nyongeza ya watu wachache bali ni kuheshimu haki za wafanyakazi wote. Papo hapo, mwengo anawaingilia katika mazungumzo yao na kuwafukuza wanaume wote. Baada ya kuwafukuza, anarudi nyumbani kwa hasira akijaribu kumwonyesha cha mtema kuni mke wake, alikuwa akimlaumu kwa umalaya uliomsukuma kuwaleta wanaume nyumbani Kwake.

Tamthilia inaishia pale tunapomwona bwana Delamon na wasaidizi wake wawili yaani Tereki na Shindo wakiuawa na wananchi. Huu ndio mwisho wa udhalimu kwa sababu wananchi wamegeuza uongozi mbaya na sasa waweza kujichagulia viongozi wa Kiafrika ambao watajali maslahi ya wananchi na kuheshimu haki zao na kurekebisha makosa ya wakoloni.

## 4.4 MFUMO WA UTAMADUNI NA JINSI UNAVYOJITOKEZA KATIKA TAMTHILIA HIZI MBILI.

Utamaduni unaojitokeza katika tamthilia mbili zilizoteuliwa ni wa mfumo dume.

AFF (2016) alifafanua mfumo dume kuwa ni mfumo uliotengenezwa maalum kwa ajili ya kumpa nguvu mwanamume dhidi ya mwanamke. Wanaendelea kueleza kwamba mfumo dume ni mfumo wa mamlaka ya kiume ambao unaendeleza ukandamizaji wa wanawake kupitia taasisi na mifumo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, kidini na kitamaduni.

Aidha, mfumo huu humpa mwanamume haki ya kutawala mwanamke katika mazingira yote kuanzia nyumbani na hata nje. Mwanamume hupewa nafasi bora ya kupata elimu Bora, kutawala na kumiliki Mali. Mfumo huu umekuwa na nguvu sana katika kuweka mipaka baina ya uwezo wa mwanamke na ule wa mwanamume katika jamii na mazingira ya tamthilia ya

kimya kimya kimya na kilio Cha haki. Mipaka hiyo haiwekwi tu katika namna wanawake na wanaume wanavyotenda Bali huwekwa hata katika jinsi ya kufikiria, kwamba fikra za mume huwa na nguvu nyingi kuliko za mwanamke (Momanyi, 2006) kwa mfano katika tamthilia ya kimya kimya kimya, Bwana Binafsi anadharau fikra za binti yake Mpya kwa kuwa yeye ni mwanamke na hatarajiwi

Wamitila (2003), alieleza mfumo dume kwa kusema mfumo wa kijamii ambao unampa mwanamume hadhi ya juu katika nyanja zote mkiwemo utawala, kiimani, kielimu na kiuchumi. Mfumo huu husababisha hali ya utumwa na ufungwa kwa mwanamke, hali ambayo huathiri ukombozi wa mwanamke kwa njia Fulani.

**4.5 Tamaduni baguzi katika elimu.**

Ubaguzi wa kijinsia katika elimu imeendelea kuwa changamoto kubwa katika baadhi ya jamii ulimwenguni. Ubaguzi wa kijinsia katika elimu unadhihirika katika baadhi ya jamii nchini Nigeria. Kwa mfano nchini Nigeria kuna chama cha wagaidi kiitwacho "boko halamu" chenye malengo ya kuhakikisha kwamba hakuna mwanamke nchini humo anayepata elimu kwa madai kwamba elimu iliyoletwa na wazungu inalenga kukiusha wanachi utamaduni wao. Kwao, mwanamke hafai Kwenda shuleni bali anafaa kubaki nyumbani, kuzaa na Kulea watoto, kutunza familia kama tamaduni zao za jadi zilivyodai (Oyaremi, 2019)

Olawunmi (2023) alituonyesha kuwa hadhi na nafasi ya wasichana katika sehemu za kaskazini nchini Nigeria ni ya chini ikilinganishwa na ile ya wavulana kutokana na mipaka hasi ya utamaduni nchini humo. Wavulana wana bahati nyingi za kupata elimu bora kutokana na mashaka ya wazazi juu ya elimu ya kike Pamoja na utamaduni hasi dhidi ya wanawake. Maoni haya yameathiri vibaya elimu ya mwanamke. Barani Africa elimu ya mvulana inapewa kipau mbele kwasababu wasichana na wanawake huonwa tu kama vyombo vya furaha vya wanaume na wazazi tu ambao kazi yao ni kuzaa na Kulea Watoto (Aleru,2018).

### 4.6 Ubaguzi kazini/umaskini.

Hope (2004) anaeleza kwamba umasikini unaweza kuainishwa kutegemea vigezo tofauti tofauti kulingana na jamii husika.kwa kwaida, umasikini ni hali ya kukosa mahitaji ya kimsingi katika maisha ya kila siku. Kwa mfano ukosefu wa lishe bora, makaazi, na hata matibabu. Mori (2014) anaeleza kwamba wanawake kazini hupaswa kugawa muda wao baina ya biashara au kazi na majukumu ya nyumbani. Mwishowe, wanawake wanajikuta hawana muda wa kutosha wakilinganishwa na wanaume ili kufanya kazi kupata pesa ambazo zingewasaidia kujikomboa kiuchumi na huu ubaguzi huchelewesha ukombozi wa wanawake kwa sababu huwaacha nyuma ya maendeleo. Kwa mfano katika tamthilia ya kilio cha haki, Lanina analaumiwa na mumewe Mwengo kwa kuacha majukimu yake ya nyumbani na kwenda kufanya kazi na kuandaa maandamano dhidi ya unyanyasaji wa bwana Delamon.

## SURA YA TANO. CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA WANAWAKE KATIKA HARAKATI ZA KULETA UKOMBOZI

### 5.1. Utangulizi

Sura hii ilichunguza misiba na changamoto zinazowakumba wanawake katika harakati za kujikomboa dhidi ya mateso. Miongoni mwa changamoto zilizoakumba wanawake ni kama vile usaliti, umaskini, ubaguzi katika elimu, matumizi mabaya ya mamlaka, unyanyasaji, migogoro na ukatili. Kama tulivyoona hapo juu, utamaduni na mipaka yake katika jamii ya tamthilia ya kilio cha haki na kimya kimya kimya husababisha kwa kiasi kikubwa uwepo wa changamoto hizi katika jamii ya wanawake.

### 5.1 Changamoto katika kazi husika.

Katika tamthilia tulizoteuwa wanawake wanakumbwa na changamoto mbalimbali katika harakati za kupigania ukombozi katika jamii zao.

## 5.2 Usaliti

Mhimili wa nadharia ya ufeministi wa kiafrika umetumia fasihi kama jukwaa ya kuelezea kwa uyakinifu hali aliyonayo mwanamke katika jamii. Mwanamke anaonekana kama mtu anayekumbana na matatizo mengi kwenye jamii. Kwa hivyo wasanii hutumia fasihi kama sehemu muhimu katika kuelezea hali na matatizo aliyonayo mwanamke kwenye jamii. Mhimili huu unatumiwa kuonyesha kuwa usaliti ni changamoto inayokumba wanawake. Wanawake katika kazi hizi wanasalitiwa na wanawake wenzao na vile vile wanaume.

Usaliti ilikuwa changamoto kubwa katika katika kujikomboa kwa mwanamke wa tamthilia ya Kimya Kimya Kimya. Kwa mfano Bw. Binafsi alimsaliti Mpya mtoto wake kwa kumufukuza nyumbani baada ya kujitokeza kutetea haki za wananchi dhidi ya uongozi mbaya wa babake. Anatendewa hivi kwa sababu amesema kuwa vitendo vya Bw. Binafsi ni vibaya na kuupinga uongozi wake. Na huo ni usaliti mkubwa kutoka kwa babake (uk.41)

> Bw. Binafsi: Shaaarab!
>
> (Anakemea. Wote wanashangaa na kunyongonyea---- Anasimama na kuchopoka kitini kwa ghafla na kuwaamrisha walinzi wake kumwendea Mpya. Walinzi wanamshika mkono na kumburura kama gunia la Mkaa!)
>
> Toka, Toka, tokaaaa. Leo, utakiramba chakula changu.
>
> Hutakunywa hata tone moja la kinwyaji changu. Sitakupa Imani yangu. Huwezi kula nguvu zangu na kunywa damu yangukisha ukanifanyia jeuri na kuonyesha hujali
>
> Toka, Toka, tokaaa.

Kwa hivyo, usaliti ni moja wapo ya matatizo yanayokumba wanawake katika harakati za kuleta ukombozi katika jamii.

## 5.3 Matumizi mabaya ya mamlaka

Viongozi wanapochaguliwa na wananchi wanatalajiwa kutumia mamlaka waliyonayo kuwatumikia wananchi wala si kuwakandamiza. Ni jukumu la viongozi kwa hivyo kuhakikisha kwamba kila mwananchi analindwa na pia anatendewa haki. Katika tamthilia tulizoteuwa,

mambo ni tofauti na haya. Kulingana na nadharia ya ufeministi wa kiafrika, popote pale, mwanamke ni mwananchi wa kiwango cha chini na anapitia kwenye dhuluma mbalimbali zinazofanywa na mwanamume na ipo haja kuirekebisha hali hii.

Katika tamthilia ya Kimya Kimya Kimya, Bw. Binafsi anatumia mamlaka yake kwa kumdharau bintiye Mpya akisema, " Wewe kigego, mtoto mkorofi, sikutaka uingie mimba mwa mamako mtoto wee. Mtoto wa kike anafaida gani? Na ilipoingia mimba sikujua kama ungezaliwa hivi wewe. Ningekung'oa mimba mwa mamako. Umekuja dunia kuniondolea furaha" (uk 34).

Pia Bw. Binafsi anatumia mamlaka yake vibaya kama mzazi na kumtendea ukatili. Kwa mfano Mpya anatendewa kikatili na baba yake hususan pale anapoita walinzi kuja na kumburura kama gunia la mkaa. Anatendewa hivi, kwa sababu amesema kuwa vitendo vya Bw. Binafsi ni vibaya nakuupinga uongozi wake. (Uk 41)

**5.4 Mateso kwa wanawake.**

Wanawake wanakumbwa na changamoto ya unyanyasaji dhidi ya haki zao katika harakati za kuleta ukombozi wa jamii.

Katika tamthilia ya Kimya Kimya Kimya Mpya alinyanyaswa na babake Bw. Binafsi kwa sababu ya kupigania haki za wananchi. Tunaona Mpya anaupinga uongozi mbaya wa babake na anatendewa kikatili na baba yake hususa pale anapoita walinzi kuja na kumburura kama gunia la makaa (uk 114).

**5.5 Hitimisho**

Katika sura hii utafiti wetu umebaini kuwa wanawake wakiwa na harakati za kuleta ukombozi, walikumbwa na changamoto mbalimbali ambazo zilinuia kulemeza juhudi zao na kufaulu. Changamoto hizi ziliwaathiri wanawake pamoja na waliokuwa wakishirikiana nao kupigana na viongozi dhalimu. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile vitisho, ukosefu wa haki, usaliti na unyanyasaji.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.0 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo ni kuchunguza utamaduni katika tamthilia ya kimya kimya kimya na kilio cha haki, changamoto zinazowakumba wanawake katika harakati za kujikomboa na kuchungungza jinsi wanawake wanavyojikomboa dhidi ya changamoto zinazowakumba wanawake. Kazi hii iliongozwa na nadharia ya ufeministi kwa kuegemea ufeministi wa kiafrika katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Utafiti huu ulitimiza malengo na matokeo kama ifuatayo.

## 6.1 Muhtasari wa matokeo

Katika sura ya nne tulichunguza suala la utamaduni katika tamthilia ya kilio cha haki na Kimya Kimya Kimya. Tulichunguza suala hili katika awamu ya baada ya uhuru. Tulieleza masuala mbali mbali katika awamu hii ambayo yalikuwa vichochezi vya kupigania ukombozi. Baadhi ya masuala haya ni kama vile ufisadi, uongozi mbaya na ukosefu wa haki. Masuala haya ndiyo kiini cha jamii zinazonyanyaswa kupata ari ya kupigania haki zao ili waweze kujikomboa.

Katika sura ya tano tulibainisha aina mbalimbali za ukombozi na jinsi wanawake wanajikomboa katika tamthilia ya Kilio cha haki na Kimya Kimya Kimya. Kulingana na utafiti huu ilibainika kwamba kulikuwepo na ukombozi wa aina mbalimbali katika tamthilia ya Kilio cha haki na Kimya Kimya Kimya. Aina hizi ni pamoja na ukombozi dhidi ya ufisadi, ukombozi dhidi ya uongozi mbaya na ukombozi dhidi ya uharibifu wa mazingira. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa palikuwepo na aina mbalimbali za ukombozi katika tamthilia tulizoteuwa. Hivyo basi wahusika wanawake wameshuhudiwa wakijitahidi kupigania aina hizi za ukombozi .

Sura ya sita ilishughulikia changamoto zilizowakumba wanawake katika kupigania ukombozi . Changamoto zilizojitokeza zaidi ni zile ambazo zilikuwa mbinu za viongozi dhalimu ambazo zilikusudia kulemaza juhudi za wanawake katika mabadiliko. Wanawake katika kazi hizi wanakubaliana na changamoto hizi bila kukata tamaa. Changamoto hizi ni kama vile usaliti, umasikini na vitisho kutoka kwa viongozi dhalimu. Vitisho hivi vinanuia kuwaita hofu wanawake ambao nia yao ni kuleta mabadiliko katika jamii zao ambazo zinanyanyaswa. Viongozi pia wanaonekana wakitumia mamlaka yao visivyo kwa nia ya kuwazuia wanawake kuendelea kupigania haki zao. Wanatumia maafisa wa polisi kuwanyamazisha wananchi na hata kuwajeruhi. Licha ya changamoto ambazo wanawake katika kazi hizi walikumbana nazo,

utafiti wetu ulibainisha kuwa wanawake hawa wakijitahidi hadi wakazikomboa jamii zao kutoka uongozi dhalimu.

### 6.2 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza suala la utamaduni na athari zake kwa ukombozi wa mwanamke katika tamthilia ya kilio cha haki ya Alamin Mazrui na Kimya Kimya Kimya ya Said A.Mohamed.

Wahusika wanawake wameangazia na waandishi mbalimbali katika kazi zao. Utafiti huu ulijikita katika waandishi wawili wa kazi za fasihi ili kujaribu kubaini mwelekeo wao na jinsi wanavyokuza wanawake katika kuleta ukombozi wa jamii zao.

Utafiti huu umeonyesha mchango mkubwa wa wanawake katika juhudi za kuleta aina mbalimbali za ukombozi kama inavyodhihirika katika kazi hii. Wanawake wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuzikomboa jamii zao kutokana na hali ngumu inazozikumba

Utafiti huu umeonyesha kuwa licha ya kuwa na wanawake wamejitahidi kuzikomboa jamii zao wamekumbwa na changamoto anuwai za kulemaza jitihadi zao. Changamoto hizi ni kama vile upinzani mkali kutoka kwa viongozi, umasikini, usaliti, vitisho na matumizi mengine. Utafiti ulionyesha wanawake wakikabiliana na matatizo haya na hatimaye wakaibuka washindi katika kuzikomboa jamii zao.

Kulingana na utafiti tulioufanya inaonekana kuna haja ya wanawake kuungana ili kujinasua na hata kunasua jamii kutoka kwa matatizo yanayozikumba. Hili limejitokeza kwa uwazi katika Kimya Kimya Kimya ambapo wahusika wengine wanawake wamejitahidi kupigana na viongozi dhalimu wanaolemaza maendeleo ya wanajamii.

### 6.3 Mapendekezo.

Utafiti ulio na manufaa ni ule ambao mtafiti anaweza kutambua pengo linaloweza kuzibwa na watafiti wengine na baadaye. Tunapendekeza ya kwamba wasomi wa baadaye watafiti kuhusu maswala mengine yanayohusiana na vyama katika kazi tofauti kifasihi.

Utafiti huu umechunguza mchango wa wanawake wa kuleta ukombozi katika tamthilia ya Kigogo na Kimya Kimya Kimya kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kiafrika. Tunapendekeza kwamba tafiti za baadaye zuchinguze nafasi ya wanawake ya kuleta ukombozi wa jamii zao katika tanzu nyingine hasa hadithi fupi, Riwaya na ushairi.

Tamthilia hizi pia zinaweza kufanyiwa uhakiki wa kimtindo kwa kuangalia jinsi kazi hizo zilivyotumia tamathali za usemi mbalimbali katika kusuka kazi zake. Hii ni kwa sababu

tulipokuwa tukichunguza tamthilia hizi tuligundua kwamba zimesheheni tamathali za usemi kama vile methali, tashbihi, kinaya, taswira na nyinginezo.

Tunapendekeza pia utafiti zaidi kufanywa kuhusiana na tamthilia hizi kwa kutumia nadharia nyingine kando ya ile ya ufeministi wa kiafrika tuliyoitumia. Kwa mfano nadharia ya uhalisia inaweza kutumiwa kuchunguza jinsi mataifa ya kiafrika yanavyolemezwa na matatizo yanayohusiana na uongozi mbaya na changamoto zinazowakumba wananchi katika harakati za kupinga viongozi dhalimu. Nadharia ya umaksi vilevile inaweza kutumiwa kuchunguza jinsi tatizo la utabaka linavyojitokeza katika tamthilia za kigogo na Kimya Kimya Kimya.

## 8.0. MAREJELEO

Dhahabu,L. L (1994). Uumbaji na Uendelezaji wa wahusika katika Tamthilia za Penina Mhando. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Fakih, S. J , (2017) Mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Utengano na Kwema si mbali Tena. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Karanja, P. M, (1990). Tamthilia za kiukombozi: Taswira ya Mwafrika katika Vita vya ukombozi dhidi ya Ukoloni. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kiango, S. ( 1992). Taswira ya Mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Tasnifu ya Uzamili; Chuo kikuu cha Nairobi.

Lugano, R. S. (1989). Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.

Mbughun, P. (1982). The image of woman in Kiswahili prose function. Makala katika Kiswahili Juzuu 49/1, uk 24. Tuki Dar- es- Salaam

Mutua , J. M. (2007). Mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.

Mwazani, E. (2015). Maudhui ya ukombozi katika Riwaya ya Vipanya wa Maabara. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.

Obure, E. (2012). Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za Rosa Mistika na Tumaini. Tasnifu ya Uzamili , Chuo kikuu cha Nairobi. ( Haijachapishwa).

Said. A. M. (2011). Kimya Kimya Kimya: Nairobi . Kenya . Longhorn Publishers.

Wamitila. K. (2004) Kamusi ya fasihi. Istilahi na Nadharia Nairobi: Focus Books.

Yego. E. K.(2013). Nafasi ya mwanamke inayohusu juhudi za mwanamke za kupinga ukandamizwaji akishughulikia nyimbo mbili za Taarabu za Zanzibar zilizotungwa na mwanamke. Tasnifu ya Uzamili.